**Learning by Ear 2009**

# Media & Information

**Author: Hope Azeda**

**Redaktion: Ludger Schadomsky**

**Kisuaheli Translation:Eric Ponda**

**EPISODE 6**

| *CHARACTERS* | |
|---|---|
| Announcer: | Male/female |
| “Young Junior” | Male, 15 years old |
| “Sister P.” | Female, 16 years old |
| “Charlie” | Male, 18 years old |
| “Ezra”: | Male, 22 years old. Brother to “Young Junior”. |
| Film Director | Adult male |

**INTRO/NARRATOR**

Hujambo na karibu tena kwa makala nyingine ya Learning By Ear tukizungumzia sekta ya Habari na vyombo vya Habari. Na iwapo ulikosa kusikiliza kipindi kilichotangulia, mambo sasa yameshika kasi baada ya Charlie,Young Junior na Sister P kumtembelea mkurugenzi wa taasisi ya mafunzo ya uandishi wa habari kujua mengi kuhusu

taaluma hiyo.Wakiwa njiani kurudi wanakutana na kundi la watayarishaji filamu na kuingiwa na hamu zaidi kutaka kujua mengi kuhusu sekta ya Televisheni.Je watabadilisha nia yao ya redio na kuingilia masuala ya televisheni?. Ungana nasi usikie yale yatakayotokea kuhusiana na uchu wao katika sekta ya filamu.

**SCENE ONE**

**Outside where the filming is taking place, there is total silence.**

1. **Film Dir:** (**Shouts) "**Kimya tafadhali". *Scene one. Take Four - and…. action".*

| |
|---|
| **SFX A clap is heard.** |

2. **Film Dir:** *Cut!* Hiyo ilikuwa sawa kabisa . Sasa tutabadilisha ***angle*** ya Kamera na nyinyi wawili mtavuka upande wa kulia na kumbuka musitazame Kamera.Sawa?

3. **Charlie:** Samahani!.

4. **Film Dir:** Ndio, unataka nini?.

5. **Charlie:** Ahh… Naitwa Charlie, huyu ni Sister P na huyu ni Junior. Sisi ni wanafunzi wageni wa idara ya uandishi katika chuo hiki.Tungependa sana kujua mengi kuhusu taaluma hii na

| | |
|---|---|
| | shughuli mnayofanya kama hilo halitakuwa tatizo kwenu. |
| **6. Film Dir:** | Sawa nitampa dakika chache tu wakati wanapopanga tena Kamera. Sasa mnataka kujua nini hasa? |
| **7. Sister P:** | Ndoto yangu ni kufanya kazi katika kituo cha televisheni, lakini sijui lolote, muda Mtu anaochukua kutayarisha kipindi. Na gani bora zaidi baina ya vyombo hivi viwili Televisheni na Redio. |
| **8. Young J:** | Pia ni gani kilicho na gharama zaidi..Redio au Televisheni?. |
| **9. Film Dir:** | Maswali hayo matatu yanaweza kuchukua muda wa siku tatu kuyajibu.Dakika chache hazitoshi. |
| **10. Charlie:** | Tutashukuru kwa ushauri wowote utakaotupa!. |
| **11. Film Dir:** | Kuhusu swali lako la ni muda gani Mtu anaweza kuchukua kuanda kipindi cha televisheni, hulo hutegemea kipindi unachotayarisha. Kwa mfano sasa hivi tunatayarisha kipindi cha mchezo wa kuigiza |

wa dakika 15, lakini imetuchukua muda wa siku 4 kufikia sasa.

**12. Young J:** Mchezo unahusu nini?... na ni kwanini imemuchukua muda mrefu hivyo?. Siku nne kwa kipindi cha dakika 15…? ni muda mrefu sana! Au ni kwasababu wahusika si wazuri?

**13. Film Dir:** Ndio na hapana .Mchezo wenyewe unahusu penzi lililoenda mrama, na muda wa kupiga picha hutegemea mazingira, mara nyingine unalazimika kutafuta meneo tofauti, mabadiliko ya hali ya hewa na masuala mengine ya kufundi .Kwa hivyo kupata picha nzuri lazima itachukua muda!.

**14. Charlie:** Ni chombo gani chenye uwezo zaidi Televisheni au Redio?

**15. Film Dir:** Kila chombo ni muhimu na kinauwezo wake, lakini mengi mutajifunza mkiwa chuoni. Binafsi hupendelea Televisheni kuliko Redio, kwani namini unaweza kusimulia hadithi kwa kina zaidi na itakayoeleweka haraka zaidi kuliko redio.Televisheni mtu anatumia macho na masikio ambavyo ni haraka kuelewa bila ya kumuacha mtazamaji na maswali mengi.Ni rahisi kutumia picha kuzua hisia zinazostahili. Binafsi na penda TV.

**16. Young J:** Na kuhusu gharama ya kuanzisha kituo cha redio ukilinganisha na televisheni?

**17. Film Dir:** (**laughs)** Huwezi kulinganisha gharama ya redio na televishni, kila kitu katika televisheni ni ghali!. Vifaa, utayarishaji na bila kusahau visanduku vya televisheni. Kwa mfano ni wangapi kijijini mwako wana Televisheni?. Sasa unaelewa namaanisha nini? Samahani muda wangu umekwsha lazima nirudi.Mbona umeshangaa hivyo. Nawatakia kila la kheri!

**END SCENE ONE**

**SCENE TWO**

**The youth centre late afternoon, the atmosphere is calm outside.**

## SFX music playing loud.

**18. Young J:** (Shouting on the top of his voice) Tuwajibike wenzangu.! Kwanini sasa munacheza badadala ya kuendelea kuandika mapendekezo?

## SFX music stops

**19. Sister P:** (**Breathless)** Unasema nini, Young J?

**20. Young:** Nauliza kwanini mnacheza badaya ya kuandika mapendekezo ya kutafuta huo ufadhili?

**21. Charlie:** (**Breathless)** Tunakusubiri wewe na Ezra. Ezra yuko wapi? Ni bora kumsubiri atupe muongozo ufaao

**22. Sister P:** Siku nyingi sijacheza.

**23. Young J:** Nimezungumza na Ezra kwa njia ya simu na ameniambia yuko njiani. Lakini mumesikia habari za hivi punde?

**24. Charlie:** Young J, wewe unaweza kuwa mwandishi mzuri sana wa habari, maana hukosi habari mpya. Haya ni habari gani hizo? Kwani waendeshaji pikipiki nchini Nigeria wamevumbua njia nyingine ya kukwepa Polisi wa trafiki?

**25. Young J:** Hapana, si mzaha…! ni jambo la kutisha hasa kwa watu kama sisi tunaopanga miradi ya kuanzisha kituo cha redio..

**26. Sister P:** Twambie basi!.

**27. Young J:** Nani ana nakala ya leo ya gazeti la ***the Focus***?

**28. Sister P:** Kwani kumetokea nini? Ofisi zao zimeteketezwa?

**29. Young J:** La hasa, hazikuchomeka, lakini wandishi wake wa habari ndio wako motoni. Wamekamatwa na ofisi zao kufungwa mara moja na na isitoshe leseni yao kufutiliwa mbali wakisubiri uchunguzi zaidi.

**30. Charlie:** Eti kumetokea nini Young J?

**31. Young J**: Wanashtumiwa kwa kuchapisha habari zinazodaiwa kutishia usalama wa taifa na pia kushirikiana na wapinzani wa serikali.

**32. Sister P:** Samahani, Young J, hebu nieleze vizuri! Yaani waandishi hao wa habari wanashtumiwa kwa kuandika uvumi?

**33. Young J:** Hapana, habari walizoandika ni sahihi, lakini lakini gazeti hilo la The Focus linashtumiwa kuchapisha habari za siri serikalini .

**34. Sister P:** Huo ni ukiukaji wa haki za binadamu na uhuru wa uandishi wa habari.

**35. Young J:** Habari hizo zilifanyiwa utafiti wa kina na kuthibitishwa kuwa sahihi. Huu ni ukiukwaji wa uhuru wa vyombo vya habari .Na kama serikali inasema ni habari za siri kwanini siri hiyo imetoka nje?. Kazi ya waandishi wa habari si ni kuelimisha umma.

**36. Charlie:** Ni mimi pia nafikiri hilo ndilo jukumu kubwa la waandikshi wa habari.

**37. Sister P:** Kwanini sasa ?

**38. Charlie:** Nilivyosikia ni kwamba Gazeti hilo lilivuka mipaka na kuandika habari zisizostahili kuchapishwa

**39. Sister P:** Hu ni upuzi. Serikali inapasa kutoa muongozo kuhusu habari zinapasa kuchapishwa. Na kufanya hivyo ni kuingilia uhuru wa uandishi huku kila siku wanapiga makelele kuhusu uhuru wa vyombo vya habari.

**40. Charlie:** Sasa nimeanza kuchanganyikiwa!.

**41. Sister P:** Kwa hivyo, Charlie, hii inamaanisha tutakapoanzisha redio yetu kuna baadhi ya habari hatutaweza kuzitangaza hata tukiwa na ushahidi wa kutosha?

**42. Charlie:** Hawa waandishi wa Gazeti la Focus walichapisha habari za kina kuhusu usalama wa taifa, vifaa vya kijeshi vinavyonunuliwa na serikali huku wakificha vyanzo vya habari hizo.

**43. Young J:** Kwani tatizo liko wapi. Wananchi wanahitaji kujua kinachoendelea humu nchini na jinsi serikali inavyotumia pesa za Umma.Waandishi wa habari wanajukumu la kufahamisha umma wakati wowote serikali inapoenda kombo.

**44. Charlie:** Hoja ya serikali ni kwamba habari hizo zilizochapishwa na Gazeti hilo la the Focus zinaweza kutumiwa na madui kuhatarisha usalama

wa taifa na hivyo ni waandishi hao wa habari watakaolaumiwa

**SFX** **Music playing again abruptly.**

**45. Charlie:** Hapana, Sister P.. !, zima huo muziki .Kwanza tujadiliane kwa kirefu kuhusiana na suala hili.

**SFX** **Music stops.**

**46. Sister P:** Nataka kucheza Muziki kwa sababu najua hatutaafikiana kuhusu suala hili. Hebu kwanza tutingishe viuno tukimsubiri Ezra.

**SFX** **Mobile phone rings.**

**47. Young J:** Hello, Hello…huyo ni Ezra? Hello…, uko mjini?

**48. Ezra:** (**phone voice)** Ndio niko mjini tunaweza kukutana kwenye mkahawa ulioko karibu na studio ya Mr T….?, unapajua?

**49. Young J:** Ndio tupatie muda wa dakika chache tu tutakuwa tumefika.

**END SCENE**

**SCENE 3**

**A busy restaurant - people and music are heard in the background**.

**SFX bottles and glasses.**

**50. Ezra:** Ehhe jamaa njooni niko hapa .

**SFX pulling chairs and sitting**

Nilihisi njaa sana. Ndio maana nikaamua nile kwanza , kwani nilijua nikifika kituoni,ni maji tu,hakuna chochote unachoweza kula !.

Ehhe, hebu niambieni, mumefikia wapi na mradi wenu wa redio?

54.Sister P: Tunajaribu kutafuta uwezekano wa kupata fedha za kununua vifaa vinavyohitajika….

55:Ezra : Wacha niwaambie kazi hiyo ya kutafuta fedha huenda ikawa ni kibarua kigumu kweli ….lakini kwa upande mwingine inaweza ikawa pia kazi rahisi..

56 Young J: Ndo sababu tunataka ushauri wako kaka.

57 Sister P: Sasa tunaanzaje?Kupata euro 20,000 unajua sio mchezo?

**58. Ezra:** Mnachohitajika kufanya ni kuandika mapendekezo kuelezea malengo yenu, na munaweza kupata

wafadhili ambao wako tayari kutoa kuwasaidia miongoni mwa jamii.Pia kuna mashirika kadhaa yanayotoa misaada kufadhili miradi ya aina hii. Lakini kwanza tuleni kisha tuendelee na mazungumzo yetu kuhusu mradi huu wa redio.

**59. Sister P:** Sawa. Charlie –Si umuulie Ezra kuhusiana na mazungumzo yetu ya awali?

**60. Ezra:** Kuhusu nini?

**61. Charlie:** Ezra... Nini maoni yako kuhusiana hatua serikali au Gazeti kuficha umma habari muhimu?

**62. Ezra:** Kwa lugha ya uandishi ni kuzuia habari muhimu.

**63. Sister P:** Maoni yako Ezra?

**64. Ezra:** Hali hii inaathiri pande zote. Serikali inaweza kutumia sheria hiyo kuwanyima raia haki ya kupata habari muhimu na si vizuri hata kidogo.

**64. Sister P:** (**laughing and jumping in her chair).** Kama nilivyotangulia kusema awali hatua hii inakusudiwa kuvikandamiza vyombo vya habari.

**65. Ezra:** Kwa upande mwengine,kwa kuzingatia sababu mbali mbali hatua hii huwa ni muhimu. Hata hivyo wakati vyombo vya habari vinaposita kutoa habari tunasema vinazuia habari hizo,lakini si rahisi

kuwaona waandishi wengi wa habari wakifanya hivyo hata wakati wanapolazimika.

**66. Young J:** Sasa kwanini nijizuie kutoa habari ambazo ninao ushahidi.

**67. Ezra:** Kwa mfano ikiwa haki ya mtu binafsi ya mwananchi wa kawaida inakiukwa kwa kuandikwa taarifa zinazohusu maisha yake ya ndani.suala pia la uhuru wa habari ni jambo ambalo linahitaji kulindwa lakini pamoja na hayo uhuru huo unakuwa ni wajibu ambao waandishi wa habari wanapaswa kuutambua.

**73.**Sister P: Sasa ni kwanini waandishi habari mara nyingine wanapuuza jukumu hilo?

**74.**Ezra : Hilo ndio tatizo mojawapo la vyombo vyetu vya habari siku hizi.Kila kituo kinataka kuwa wa kwanza kutangaza habari Fulani zinazochipuka,mara nyingi vituo hivi havifikirii matokea ya hatua hiyo…..

**75,Charlie:** Mimi pia nimefikiria jambo hilo….

**76. Ezra:** Mfano mzuri, mara nyingine unapotazama habari katika televisheni, hutakosa kusikia habari zinazogusia masuala ya uchunguzi unaoendelea na hii ni kinyume cha sheria na maadili ya uandishi wa habari. Kwani habari hizi zinaweza kuathiri kesi inazoendelea ambapo mshtakiwa huenda

asitendewe haki. Idara ya sheria inaweza kutumia habari hizi na haipasi kuzingatia uvumi hadi pale mshtakiwa atakapopatikana na hatia lakini utakuta mara nyingi hali sheria hii haizingatiwi na vyombo vya habari.

**77. Sister P:** Ehehe wenzangu tunawezakupata chakula? Nahisi njaa na mazungumzo haya yanaweza kuendelea kwa muda mrefu.

**(shouts)** Mhudumu….!

**END OF EPISODE**

**OUTRO/NARRATOR**

Na hadi hapo ndipo tunapofika mwisho wa makala haya ya leo kuhusu taaluma ya uandishi na Vyombo vya Habari. Usikose kungana nasi wakati mwengine kwa makala mengine ujue yanayoendelea kwa wanahabri hawa chipukizi ambao sasa wameanza harakati kutafuta fedha za kufadhili mradi wao. Ukiwa na maoni unaweza pia kuwasiliana na kundi la Noa bongo jenga maisha yako mjini Bonn, kupitia mtandao wetu wa dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.